



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ASASI ZA KIRAIA ZILIZOPATA KIBALI
CHA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA WAKATI WA UCHAGUZI MDOGO
WA UDIWANI KATIKA KATA 23 TANZANIA BARA

Dodoma, 24 Februari, 2024

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 24 Februari, 2024, imetoa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi mdogo wa Udiwani katika kata 23 za Tanzania Bara kwa asasi za kiraia 11. Tume imefikia uamuzi huo kwa kuzingatia kanuni ya 3 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, inayoipa Tume jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo. Orodha ya asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na maeneo watakayotoa elimu hiyo, imeoneshwa katika jedwali lifuatalo:-


NA.	JINA LA ASASI YA KIRAIA	HALMASHAURI	KATA
1.	Mbogwe Legal Aid Organization (MBOLAO)	Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe	Isebya
2.	Sustainable Hub for Policy Initiatives (SHPI))	Halmashauri ya Manispaa ya Musoma	Mshikamano
		Halmashauri ya Wilaya ya Butiama	Busegwe
3.	Promotion and Women Development Association (PWDA)	Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji	Kasingirima
4.	Bagamoyo Community Capacity Empowerment and Education (BCCEE)	Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo	Fukayosi
5.	Action for Democratic Governance (A4DG)	Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	Kimbiji

NA.	JINA LA ASASI YA KIRAIA	HALMASHAURI	KATA
6.	Vanessa Foundation	Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	Nkokwa
7.	Tanzania Centre for Disability Development Initiatives (TCDDI)	Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	Nkokwa
8.	Safe Society Platform Tanzania (SSPT)	Halmashauri ya Wilaya ya Butiama	Busegwe
		Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe	Isebya
9	Youth Against Aids and Poverty Association (YAAPA)	Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji	Kasingirima
10	Musoma Municipal Paralegal Organisation (MMPO)	Halmashauri ya Manispaa ya Musoma	Mshikamano
11	Shirika la Elimu ya Uraia na Uzalendo "Civic Education and Patriotism Association"	Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	Kimbiji
		Halmashauri ya Mji Kibaha	Msangani
		Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo	Fukayosi
		Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	Mlanzi
		Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	Kibata

Aidha, katika utekelezaji wa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura, asasi hizo zitapaswa kuzingatia Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa Mwaka 2020 katika kipindi chote cha kutoa elimu hiyo katika uchaguzi mdogo.

Tume inatumia fursa hii kuzipongeza asasi zote za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura. Vile vile, Tume inazikumbusha asasi za kirai zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi chote cha uchaguzi.

Imetolewa na:



MKURUGENZI WA UCHAGUZI